

## **Dhima ya Viakifishi katika Ushairi Huru wa Kiswahili**

*Joseph Nyehita Maitaria*  
*Chuo Kikuu cha Karatina, Kenya*

### **Ikisiri**

Ushairi, kama zilivyo tanzu nyingine za fasihi, huwasilishwa kwa matini za lugha zilizoakifishwa ili kuelekeza usomaji, uwasilishaji wa kimantiki, kubainisha zaidi matini zilizotumika na kuondoa utata katika fasiri za jumbe kusudiwa. Washairi hutumia viakifishi kama mtindo na mbinu ya kibinafsi katika uwasilishaji. Hata hivyo, kuna aina mbili za matumizi ya viakifishi katika uwasilishaji wa tanzu za fasihi: Kwanza kuna matumizi ya ‘kawaida’ ambayo ni utaratibu unaofahamika miongoni mwa watunzi. Aghalabu matumizi haya yanajitokeza zaidi katika tungo za mashairi zinazingatia mno arudhi katika uwasilishaji. Pili, kuna matumizi ya ‘makusudi’ ya viakifishi ambayo yanabainika zaidi katika uwasilishaji wa mashairi ya Kiswahili yanayowasilishwa kwa kutozingatia mno arudhi za utunzi. Kutokana na uwepo wa njia hizo mbili za uwakifishaji, kuna haja ya kufafanua na kufasiri dhima ya viakifishi katika ushairi wa Kiswahili. Makala hii inafafanua namna watunzi wa ushairi huru wa Kiswahili wanavyotumia viakifishi kama mtindo na mbinu elekezi katika kuwasilisha hisi, ubainishaji wa ujumbe na ujenzi wa muktadha wa usomaji. Mifano itatokana na baadhi ya mashairi katika diwani za Kichomi(E. Kezilahabi) na Bara Jingine (K. Wa Mberia). Mwishowe, imependekezwa namna viakifishi vinavyoweza kutumiwa kwa ufaafu zaidi katika uelekezaji wa taratibu za usomaji na uwasilishaji wa ujumbe katika mashairi ya Kiswahili.

Maneno Muhimu: Dhima, Viakifishi, Ushairi Huru

### **Utangulizi**

Ushairi ni utungo wa fasihi unaowasilishwa kwa namna mbili: kisimulizi na mshikamano kimaandishi. Unapowasilishwa kimaandishi, matini huakifishwa ili kujenga ushikamano wa maumbo, miundo na wakati uo huo kuelekeza utaratibu wa usomaji wa mashairi. Uwasilishwaji wake hutumia lugha ya mkato yenye kuelezea maudhui kwa muhtasari na kuyaficha ndani ya taswira na ishara (Senkoro, 1987: vii; Harries, 1962: 272). Miongoni mwa ishara hizo ni viakifishi. Azma ya uakishaji ni kuziratibu matini zilizotumiwa ili kuondoa utata wa kimawasiliano unaoweza kuwepo katika ufasiri wa ujumbe. Kadhalika, ushairi Kiswahili una historia ndefu kwa kuzingatia dhima yake katika jamii na pia kupitia kwa mbinu teule zinazojikita katika

fani, umbuji na maudhui (Mulokozi na Sengo, 1995). Hii inatokana na namna mtunzi anavyoteua na kupanga mizani (au silabi), maneno, mishororo (au mistari) katika beti za shairi. Kulingana na Mboya (2000) na Mulokozi na kahigi (1978), shairi ni utungo unaozingatia utaratibu maalum wa maneno teule yenye muwala na lugha ya mkato yenye mahadhi ili kuelezea tukio au hisia za mtunzi. Kimsingi, viakifishi husaidia uwasilishaji wa matini kwa kuzingatia kanuni za kisarufi (Wanjala na Kavoi, 2013; Kitsao, 1995). Ingawa utaratibu huo ni muhimu katika ubainishaji wa sifa za tungo za mashairi ya Kiswahili, viakifishi ni uti wa mgongo katika ubainishaji wa matini husika katika uwasilishaji, uelekezaji wa usomaji wa kimoyomoyo na kughani kwa sauti. Kabla ya majilio ya hati za maandishi katika Afrika Mashariki, mashairi ya Kiswahili ya asili yalikuwa yakighaniwa. Kimsingi, ushairi huo ulitungwa kwa kuzingatia mapigo ya sauti (Macgoye, 2009: 17). Katika muktadha huo, baadhi ya vielekezi muhimu katika fasiri za mashairi hayo ni kuzingatia mahadhi, mikazo inayotumiwa katika maneno na kauli, ukariri wa maneno au kauli zinazotumiwa (uradidi), kupanda na kushuka kwa sauti (kiimbo) wakati wa usomaji wa kimoyomoyo au wa sauti, jinsi miundo ya maneno yanavyofanyiwa marekebisho ya makusudi (mazida na inkisari) na mihemko katika uwasilishaji. Vielekezi hivi vianabainika zaidi katika ushairi simulizi.

Kwa sasa katika uwasilishaji wa mashairi ya Kiswahili, matumizi ya viakifishi hushikilia nafasi muhimu. Washairi wa Kiswahili wamekuwa wakitumia viakifishi kwa namna mbalimbali ili kukidhi malengo ya usomaji na ufafanuzi wa maudhui. Kuna aina mbili za matumizi ya vikifishi katika uwasilishaji wa mashairi ya Kiswahili: Kwanza ule uakifishaji wa ‘kawaida’<sup>1</sup>. Matumizi hayo yanajitokeza zaidi katika tungo za mashairi zinazozingatia ‘sheria’ au arudhi katika uwasilishaji. Mashairi hayo yanaweza kughaniwa au kuimbwa kutokana na uwepo wa mizani na vina katika uwasilishaji wake (Alembi, 2000). Kadhalika, kuna uakifishaji wa ‘umakusudi’<sup>2</sup> ya viakifishi unaobainika zaidi katika uwasilishaji wa mashairi huru ya Kiswahili. Hata hivyo, mashairi yawe yanatumia viakifishi kwa ‘kawaida’ ama kwa ‘makusudi’; hayajapwelewa au kutindikiwa katika udhibiti, ubainishaji na uwasilishaji wa ujumbehusika. Kwa mantiki hii, kuna haja kufafanua sababu zinazowafanya watunzi wa ushairi wa Kiswahili kutumia viakifishi kwa namna hizo mbili.

Makala hii inafafanua namna watunzi wa ushairi huru wa Kiswahili wanavyotumia viakifishi kama mbinu na mtindo katika kuibulia hisia, ubainishaji wa ujumbe na ujenzi wa muktadha elekezi katika usomaji wa tungo hizo. Miongoni mwa watunzi wasifika katika kitengo cha ushairi huru wa Kiswahili ni C. Hauli, E. Hussein, E. Kezilahabi, F. E. M. K. Senkoro, H. Muhanika, J. Angira, K. wa Mberia, K. K. Kahigi, M. M.

---

<sup>1</sup> Huu ni uwasilishaji kwa hati za maandishi kwa kunaozingatia taratibu zifahamika katika uwasilishaji wa matini.

<sup>2</sup> Huu ni uwasilishaji katika uandishi unaobinafsisha vipengele vinavyotumika katika uwasilishaji wa matini.

---

Mulokozi na T. Mvungi. Katika kundi hilo pia wapo watunzi wengine waliojitokeza na tungo zenye mwelekeo huu kama vile K. Wamitila (2004), M. Khatib (2003), S. A. Mohamed (2002) na A. Mazrui (1994). Katika makala hii, mifano itatokana na baadhi ya mashairi yanayopatikana katika diwani mbili: *Kichomi* (E. Kezilahabi) na *Bara Jingine* (K. Wa Mberia).

### Viakifishi katika Uwasilishaji wa Matini za Ushairi

Katika usomaji wa fasihi andishi, hakuna njia nyingine ya kuupokea ujumbe ila kupitia kwa matini zilizoakifishwa na kutumiwa na mtunzi. Katika mashairi, viakifishi mbalimbali vimekuwa vikishirikishwa katika kubainisha na kueleza waziwazi ujumbe kwa madhumuni ya kuwasiliana na hadhira kwa thamani ile ile inayokusudiwa na mtunzi. Kwa uelekezi wa viakifishi, matarajio ya mtunzi ni kuwa, ujumbe utakuwa unaifikia hadhira ili isiwe na namna nyingine ya ufasiri. Hivyo, hadhira inaelekezwa katika usomaji na kutambua aina mbalimbali za kauli zinazotumiwa katika uwasilishaji wa mawazo katika utungo. Katika mawasiliano yanayotumia hati za maandishi, viakifishi ni muhimu katika kuondoa utata usiokusudiwa, ubainishaji wa kauli na kuhakikisha kuwa ujumbe umesafirishwa kwa njia inayastahili. Miongoni mwa viakifishi ambayo hutumiwa na watunzi wa ushairi katika uwasilishaji wa tungo ni nukta [·], nukta mbili [∴], mkato au koma[|], alama ya mshangao[!], alama ya kuuliza[?], mabano au paradesi [( )], alama za usemi au mtajo[" "] au [' ’] kistari kirefu [—], kinyota[\*], kistari kifupi [-], ritifaa [’], nukta za dukuduku [...] na nukta na mkato [;]. Kadhalika, kuna matumzi ya herufi kubwa, herufi za mlazo au italiki, na herufi kwa wino uliokoza. Vipengele hivi hutumika ndani kwa ndani katika beti zilizopo, kwenye kingo zake au mwishoni mwa shairi linalowasilishwa. Kuna uwezekano wa kutumiwa kwa viakifishi zaidi ya kimoja katika mazingira yayo hayo. Baadhi ya mashairi huzingatia pia vipengele vya uchapaji kimuundo<sup>3</sup> kama vile kuacha mwanya mpana mwishoni mwa ukwapi na mwanzoni mwa utao, mpangilio wa maneno kulingana na vitendo (Tazama neno ‘*iliporiomoka*’ kwenye shairi ‘Mruko wa Nyuki’ katika *Bara Jingine*. 23). Kwa hivyo, katika mashairi huru viakifishi vinavyotumiwa vinachangiwa mno na grafolojia ya uwasilishaji.

Mashairi ya Kiswahili yawe ni yale yanayozingatia arudhi au mashairi huru, yote yanatumia viakifishi katika uwasilishaji wake. Hata hivyo, viakifishi hivyo huweza kutumiwa labda katika kutimiza mahitaji ya kikaida ya kiuwasilishaji ama vinaweza kubinafsishwa ili kumhudumia mtunzi wa ushairi wa Kiswahili. Kama vile ilivyoelezwa hapo juu, baadhi ya watunzi huweza kutumia zaidi ya kiakifishi kimoja katika sehemu hiyo hiyo moja. Kinachoelekeza aina ya matumizi hayo huweza kuwa mtindo ama aina ya ujumbe unaowasilishwa. Hapa ieleweke kuwa kila kiakifishi

---

<sup>3</sup> Haya huzingatia katika michakato ya uchapishaji labda kwa kuzingatia uelekezaji wa wani mahitaji ya ushairi au kwa uelekezi wa kibinafsi wa mtunzi (Pia hujulikana kama miundo ya *kigrafolojia*)

hukaulishwa katika kutekeleza dhima ya uwasilishaji wa shairi kulingana na azma ya mtunzi. Kadhalika, kuna viakifishi ambavyo ni vya lazima au ‘vya kawaida’. Ukawaida huu hujitokeza mno katika mashairi yanayozingatia zaidi arudhi za uwasilishaji kama inavyodhihirika kwenye shairi la ‘Jipu’ katika *Sauti ya Dhiki* (Abdalla, 1973: 7-8):

Towa taka masikiyo, upulikize uneni  
Haya upulikizayo, uyatiye akilini  
Kwani ni muhimu hayo, wendapo utabaini  
Kwa hivyo fanya makini, upate kuyasikiya (ubeti wa 1)

Katika ubeti huo, kiakifishi cha [J] kimetumiwa kukidhi mahitaji ya mwisho ya kina cha ndani (ukwapi). Katika kina cha mwisho au kwenye kingo zake hakuna kiakifishi chochote. Kwa upande wa uwasilishaji wa mashairi huru, ukawaida huo unaweza kukiukwa kwa ‘makusudi’ kwenye shairi la ‘Karamu za Kadimu’ katika *Jicho la Ndani* (Mohamed, 2002: 82):

Kadimu hali kadimu	wala vinyama vikofu
Hula mitamba ya nyama	minoo mitononofu
Shahamu za kugandama	kwenye kina cha minofu
Mifupa huisukuma	kwa walio watwalifu
Peleleza utaona!	(Hili ni shairi zima)

Shairi hilo hapo juu halikutumia viakifishi vya ndani kama inavyobainika kwenye shairi la ‘Jipu’. Huenda mtunzi hakutaka kutumia kiakifishi hicho cha [J] ambacho kimekuwa kikitumiwa kwa mtindo uo huo kwa muda mrefu. Badala ya kutumia kiakifishi hicho, mtunzi ameacha mwanya kutekelezea dhima ya kiakifishi hicho. Maelezo hayo yanaweza kuashiria, kwa kiasi fulani, namna mashairi yanayozingatia arudhi zaidi yanavyotofautiana na mashairi huru ya Kiswahili kwa upande wa matumizi ya viakifishi.

### Uakifishaji wa Mashairi Huru

Vipengele katika uakifishaji ni vingi na kila kimoja hutumiwa kutekelezea dhima fulani mahususi au vikiwa ni viwili huchangiana katika kuubainisha na kuuwasilisha zaidi ujumbe unaowasilishwa. Vipengele vya viakifishi hutumiwa katika uwasilishaji wa matini, hususan katika mashairi ya Kiswahili kama utanzu mmoja wa fasihi andishi. Kama vile ilivyoelezwa hapo awali ni kwamba mashairi yoyote yale (bora yamewasilishwa kwa maandishi), viakifishi huzingatiwa kwa uwazi au hufichwa katika grafolojia. Baadhi ya maswali ambayo yanaweza kuzingatiwa katika kubainishia dhima ya viakifishi katika mashairi huru ya Kiswahili ni yafuatayo.

- i. Ridhimu na mizani katika mashairi huru ya Kiswahili hudhibitiwa vipi kupitia kwa viakifishi vilivyopo?
- ii. Viakifishi katika mashairi huru ya Kiswahili huelekeza usomaji wa hadhira?

- iii. Dhima ya viakifishi tofauti vinafanana na kutofautiana vipi katika uwasilishaji wa toni katika mashairi huru?
- iv. Ughanaji tofautitofauti wa mashairi huru ya Kiswahili huweza kuwa ni matokeo ya fasiri tofauti za viakifishi?
- v. Usaili na utafakari wa mashairi huru huweza kuelekezwa vipi kupitia kwa viakifishi?
- vi. Viakifishi huambatana vipi katika kuibulia hisia za watunzi wa mashairi huru ya Kiswahili?
- vii. Usaili na utafakari huwezaje kuelekezwa kwa viakifishi vilivyomo katika mashairi huru ya Kiswahili?
- viii. Kiwango gani cha ufahamu ambao msomaji anahitaji kuwa nao katika kutambua aina ya viakifishi vinavyoshirikishwa katika uwasilishaji wa ujumbe katika mashairi huru ya Kiswahili?
- ix. Uhuru wa kimbuji wa washairi huru wa Kiswahili huweza kujitokeza vipi kupitia kwa viakifishi vilivyotumiwa?

Maswali ambayo yamedokezwa hapa yanaweza kusaidia katika uhakiki wa mashairi huru ya Kiswahili. Maswali haya yanaweza kuwa mwongozo katika kufahamu dhima inayotekelezwa kupitia kwa viakifishi vinavyotumiwa katika uwasilishaji wa mashairi. Kadhalika, maswali hayo yanaweza kutumiwa katika kutathmini uwiano uliopo katika mtunzi, hadhira na muktadha ulioibua utungo huo.

### **Matumizi ya Viakifishi katika Mashairi Huru ya Kiswahili**

Katika uwasilishaji wa fasihi andishi kuna viakifishi mbalimbali vinavyoweza kutumika kama vile vilivyorejelewa hapo awali. Viakifishi hivyo hutumiwa kwa malengo mbalimbali. Katika mashairi huru ya Kiswahili, viakifishi hutumiwa kwa dhima mbalimbali kama inavyoelezwa hapa.

#### **i. Taratibu za Kisarufi**

Matarajio ya mtunzi wa shairi huru ni kuwa, shairi alilolitunga litawasilishwa, kupokelewa na kufasiriwa kulingana na lile alilokusudia. Kielekezi hapa ni namna mtunzi alivyotumia vipengele vya viakifishi vilivyotumiwa. Aidha, namna viakifishi vilivyotumiwa katika mashairi haya ni njia mojawapo ya kuwabainisha watunzi ambao wanafahamu vizuri lugha hii ya Kiswahili na namna inavyofanya kazi. Mfano unaoweza kuzingatiwa ni shairi la ‘Mwamba Ziwani’ katika *Kichomi*(Kezilahabi, 1974). Shairi hilo limewasilishwa hivi:

Hautingishiki, hauzungumzi, umekufa;

Lakini ninaweza kuusikia ukizungumza;

“Kijana mimi sicheki, uwe hivyo na wewe.

Tazama jinsi ndege walivyokifanya kichwa changu

Cheupe kama mchwa wa fuvu, mimi nimetilia,

Sina wasiwasi inagwa naonekana mjinga,  
Mawimbi yananigusa na kuvunjika  
Kama upanga wa muuaji ushindwavyo kawa roho,  
Mimi ni imara na sitingishiki,  
Na mtu mwovu siumuziki.” (uk. 6)

Dondoo la shairi la ‘Mwamba Ziwani’ lililorejelewa halijatumiwa mgawanyo wa beti katika uwasilishaji wake lakini limebainisha namna mbalimbali za matumizi ya viakifishi ambavyo vinaelekeza utaratibu wa masuala ya sarufi. Ingawa sehemu hii ya shairi imewasilishwa kwa mishororo ambayo inaweza kusomeka na kueleweka kwa kuzingatia viakifishi vilivyotumiwa. Viakifishi vilivyotumiwa katika uwasilishaji wa sehemu ya awali ya shairi hilo (Tazama wino uliokoza uliotomewa viakifishi katika dondoo la shairi hapo juu). Viakifishi hivyo vinasaidia kuifanya matini ya shairi hili kuweza kueleweka kisarufi. Kwa mfano, katika mshororo wa awali ‘Hautingishiki, hauzungumzi: umekufa;’ kumetumiwa viakifishi sita: herufi kubwa, mkato, nukta na mkato, alama za usemi/mtajo, mkato/koma, nukta mbili na nukta. Kila kipengele kimetumika katika uelekezaji wa usomaji. Kwa maelezo ni kwamba, **Herufi Kubwa** zimetumiwa kuonyeshwa mianzo katika mishororo; ishara ya [.] imetumika katika kufahamisha uorodheshaji na kutenganisha mfululizo wa matukio; [:] inaashiria kutenganishwa kwa hoja kuu ya awali kabla ya kifungu au maelezo mafupi yanayohitajika; nukta na mkato [;] ni ishara ambayo inaashiria kuwa neno au hoja nzito inahusiana kwa namna moja na ile iliyotangulia, inaweza pia kuwa kashiria kinachounganisha hoja hizo mbili zinazofuatana; [.] imetumiwa kuashiria miisho ya kifungu au ukamilifu wa hoja; [“ ”] ni ishara inayoonyesha dondoo maalum au kauli ambayo si ya mtunzi na huenda ikawa ni ya mtu mwingine. Kauli inaweza kuchukuliwa kama utanzu ndani ya utanzu au matini moja ndani ya matini nyingine. Katika muktadha wa viakifishi hivyo, azma ya mtunzi ni kuelekeza zaidi usomaji wa hadhira kwa kuzingatia taratibu za kisarufi. Kwa mfano, katika matumizi ya [“ ”], mtunzi anadokeza kuwa hiyo si kauli yake na pia anaitaka hadhira kukabiliana na matini hiyo kwa nafsi ya mwingine. Kwa kutumia kiashiria hiki usomaji hautarajiwi kuwa na viwingu vya utata ambapo nafsi mbili: ya mtunzi na kauli za wengine zitakuwa zinadhitiwa. Kutokana na viakifishi, ushikamano na mahusiano ya maneno; miundo ya mizani au kauli katika shairi huwasilishwa kwa kufungamanishwa na kaida za kisarufi.

## ii. Viakifishi kama Njia ya Kujenga Uhuru katika Usarifu Lugha

Kutokana na matumizi ya viakifishi, mshairi amejipa uhuru wa kusarifu, kuitawala na kuidhibiti miundo ya lugha ili kuweza kumtumikia jinsi apendavyo katika uwasilishaji hoja na matukio. Uhuru wa msanii katika kuisarifu lugha katika uwasilishaji wa utungo wake unaweza kufafanuliwa kupitia shairi ‘Nimechoka’ katika *Kichomi*, uk.34). Katika shairi hili imewasilishwa:

Mikono inaniuma, na waya imekwishanikata vidole,  
Damu imetiririka hadi kwapani; kujipangusa siwezi.

Nimechoka, Kadri niendelezavyo kuning'inia, ndivyo  
Sura yangu ionyeshavyo vizuri alama za uchovu.  
Ninatazama huku na huko kuwatafuta wenye huruma,  
Lakini wanadamu wote wazima wanainamisha vichwa  
Chini kama kwamba hawanijui; hata jamaa zangu! (Ubeti wa 3)

Katika ubeti huo uliozingatiwa hapo juu, mshairi ametumia viakifishi mbalimbali. Ubeti huu umetumiwa viakifishi kama vile: **Herufi Kubwa [,], [;] na [.] [!]**. Katika uwasilishaji mshairi ametumia kikomo kama njia ya kutenganisha mfululizo wa matukio na wala si ishara ya kubainishia vina katika ukwapi na utao kwenye mishororo. Hii ndiyo sababu ameitumia ishara hiyo ya [,] baina ya 'inaniuma, na'. Hata hivyo, matumizi hayo yametokea katika mkabala wa kiunganishi kingine cha 'na' ambapo msanii anaitarajia hadhira yake kwanza izingatie athari ya maumivu ya 'mikono' kisha athari ya 'waya' ambao tayari umekwisha kama. Kwa hivyo, ishara ya [,] imetumiwa kwa makusudi katika mshororo huo. Mfano huu pia unashabihi ule unaopatikana katika mshororo wa kwanza na wa pili. Isitoshe, swali la kujiuliza hapa ni: Kwa nini mshairi hakutumia viakifishi vyovyote katika mishororo? Mshairi alikuwa na makusudi fulani, kwamba, angependa mishororo hiyo isiyokuwa na viakifishi katika miishio yake inahitaji kukamilika katika mishororo inayofuatia. Kipengele cha [!] kuibadili kauli iliyopo kuwa ya mshangao kama hangetumia kiakifishi hiki, yangekuwa kuwa maelezo tu ya kawaida. Kadhalika, kutokea kwa [!] mwishoni mwa ubeti inatekeleza mambo matano. Kwanza, kama kimalizio katika ubeti, hoja iliyokamilika, kuchochea usaili na tafakari na pia kama mbinu ya kujengea taharuki ili kubainisha mwisho wa ukwapi, hadhira nayo huweza kuhisi athari yake wakati wa usomaji wa shairi. Mwelekeo huo wa usarifu lugha umekuwa ukitumiwa na watunzi wa ushairi huru inavyodhihirika katika uwasilishaji wa shairi 'Hasira Hasara?' katika *Chembe cha Moyo* (Mazrui, 988: 23). Shairi hilo limewasilishwa ifuatavyo.

Ayi, Hasira, uweje kwangu hasara  
iwapo dhuli ndiyo yangu tijara  
ilonishambulia ja simba marara  
ikanichanachana kama tambara  
Basi Hasira, kwangu uweje, Hasara? (Ubeti wa 1)

Katika shairi hilo mshororo wa mwisho unazingatia dhima kama ile inayotekelezwa katika shairi 'Nimechoka' lakini tofauti ni katika viakifishi hivyo viwili. Katika shairi hili kiakifishi [?] kimetumiwa katika kuisarifu zaidi methali 'Hasira ni Hasara' kwa kuifanyia marekebisho ya kiasi katika kuidondosha silabi ya 'ni' na kuwa 'Hasira Hasara?' hayo yanafanywa katika kauli ya kimalizio kwa kutumia herufi kubwa katika 'Hasira' na 'Hasara' na kwa kutumia kiakifishi [?] kunaivua methali ule ukauli na kuifanya kuwa swali la kuchochea tafakari.

### iii. Viakifishi kama Mbinu ya Kuwasilisha Mawazo

Katika tungo za fasihi hususan katika ushairi, ujumbe unaowasilishwa unahitaji kuifikia hadhira na huchukuliwa kuwa muhimu. Hata hivyo, ujumbe huo huwasilishwa

kupitia kwa lugha inayotumiwa kwa makusudi na mshairi. Isitoshe, viumbiumbi vya lugha vinavyotumiwa vinahitaji kuratibiwa ili kuweza kuwasilishwa kwa utaratibu unaozingatia viakifishi. Katika muktadha huo, ujumbe huwasilishwa kwa mantiki, muhtasari na hatua kwa hatua ili kusiwe na namna nyingine ya kuufasiri. Hivyo, mshairi hutumia viakifishi katika kujenga na kuelekeza mawazo yake. Matumizi mwafaka ya vakifishi humfaidi mtunzi wa ushairi ili kuwa na dira ya uwasilishaji wa mawazo. Kama vile ilielezwa hapo awali vipengele vya uakifishi ni vingi mno na mshairi huteua vile ambavyo vinaweza kumsaidia katika kusafirishia mawazo yake. Viakifishi hivyo hutokea kwenye kingo, ndani na hata mwishoni mwa ubeti au shairi linalozingatiwa (Tazama mifano ya beti za mashairi yaliyozingatiwa hapo awali na ile inayoyotolewa hivi punde). Baadhi ya vipengele viakifishi huwa na sifa ya kujitokeza mwanzoni, katikati au ndani na mwishoni mwa mashairi huru ya Kiswahili. Aidha, matumizi ya viakifishi husaidia kuingia katika kiini cha ujumbe wake bila ya kupoteza muda. Kwa sababu, viakifishi kama ishara huweza kufasiriwa na vile vile ujumbe unaowasilishwa kumuktadhishwa katika uhalisi wa maisha na tajiriba ya hadhira katika jamii. Mfano hapa ni shairi ‘Mafahali wapigana’ katika *Kichomi* (uk. 5). Mshairi anawasilisha:

Mafahali wenye matumbo wanapigana,  
Chini, chini, chini zaidi  
Mpaka vichwa vyaovinagusana[.]  
Halafu watazamaji wakondefu  
Wanaanza kupiga kelele,  
Haya! Haya! *Machakulo*\* haya!  
Pole pole hawaoni kitu,  
Vumbi hewani, vumbi machoni,  
Vumbi kuisha, mshindwa amekwisha kimbia,  
Mshindi juu ya kichuguu amekaa,  
Akionyesha kidole kimoja sasa  
Mchwa ndio askari. (Ubeti 1)

Ubeti huo ni wa awali katika shairi. Kwa kuzingatia viakifishi vilivyotumiwa, mtunzi amepania kuwasilisha mawazo yake hatua kwa hatua. Mishororo imejitokeza kiawamu ambapo ule wa kwanza ni kauli ya kutanguliza mawazo yanayowasilishwa. Hili linadhihirika kupitia kwa mambo mawili: **Herufi Kubwa** mwanzoni na mwishoni mishororo kumetumiwa [.] Katika muktadha wa ubeti huo, mishororo huo ni kauli inayotanguliza, na kuwa kama dibaji ya kisa kinachosimuliwa. Baada ya utangulizi huo, msanii anaanza kwa kuelezea kwa mfululizo kisa kinachoweza kushuhudiwa katika uhalisi wake ambapo ‘Mafahali wenye matumbo’ ndio wanaopigana. Mfululizo wa matokeo haya yanaelezwa kwa matumzi ya [.] ambazo ni mbili kutenganisha maneno matatu yayo hayo. Hii inamaanisha kuwa, mtunzi anatarajia tukio na vitimbi hivyo kuweza kufuata bila utata hadi katika neno ‘vinagusana’ ambapo kuna kiakifishi [.] Hata hivyo, inabainika kuwa mianza ya mishororo yote katika ubeti ni **Herufi Kubwa**. Kilelekezi hapa ni kuwa mishoro hiyo ni ya muhimu na wala haipaswi



kupuuzwa. Kadhalika, mianzo hiyo inweza kuwa ya viwango sawa; ile yenye kupewa uzito zaidi ni ile ambayo inaanza hoja ambayo inahitimishwa kwa kiakifishi [·]. Katika kujenga muktadha ambao huenda usieleweke kwa hadhira, mtunzi ametumia neno lenya asili ya kigeni *Machakulo*\* ambalo limewekewa **Kinyota** mwishoni na maelezo kutolewa mwishoni mwa shairi. Zaidi ya kwamba, mashairi huru ya Kiswahili yanawasilishwa (hasa) kwa kuzingatia Kiswahili sanifu na pindi maneno ya kigeni yanapojitokeza; mtunzi hana budi kutoa ufafanuzi unaostahili. Hivyo, watunzi wa mashairi huru huwasilisha mawazo kwa hadhari zaidi na huhakikisha kuwa habakishi mianya ambayo inaweza kuzua utata katika usomaji na upokezi wa ujumbe. Kwa njia hii ya utumiaji wa viakifishi mwafaka, husaidia katika kuhakikisha kuwa mawazo yametiririshwa kimantiki kutoka mshororo mmoja hadi mwingine na ushikamano wa ubeti na ubeti katika shairi.

#### iv. Viakifishi katika Kuchochea Usaili na Utafakari wa Ujumbe

Viakifishi katika ushairi huru wa Kiswahili huwa chombo cha kujengea muktadha wa kufumbia fumbo ambapo mtunzi hutumia katika uwasilishajiwa kazi yake. Kadhalika, ujumbe unaowasilishwa huwa si wa moja kwa moja kwa hadhira isipokuwa pale ambapo imekusudiwa na mshairi. Hivyo, viakifishi ni vipengele vya kuchochea usaili na utafakari. Hapa ieleweke kuwa idadi ya viakifishi katika uwasilishaji wa mashairi haya hutegemea malengo na athari inayokusudiwa katika upokezi wa hadhira. Hapa kuna madondoo ya beti mbili zinazozingatwa: shairi ‘Machozi ya Damu’ katika *Bara Jingine* (uk. 1) na shairi ‘Wanafiki’ katika *Kichomi* (uk. 24). Katika ‘Machozi ya Damu’ imewailishwa hivi:

Majuto ni mjukuu;  
Tulipochezea kinamo  
Katika karakana ya siasa  
Hatukujua kwamba vinyago  
Vimejibadilisha maumbile  
Na kujigeuza miungu\_wajeuri  
Matumalize machozi ya damu  
Kwa kutuzamisha kucha  
Hadi mafundo ya neva! (Shairi kutoka *Bara Jingine*, uk. 1)

Katika shairi ‘Machozi ya Damu’, mtunzi ametumia viakifishi vichache katika uwasilishaji wa shairi hili. Hata hivyo, viakifishi viwili vinaporejelewa: [·] na [!] ni kwamba, vimetumiwa katika sehemu mbili muhimu; katika mshoro wa ufunguzi wa shairi na katika mshororo wa kuhitimsaha shairi. Katika mshororo wa kwanza kumetumiwa ‘Majuto ni mjukuu:’ na katika mshororo wa mwisho ni: ‘Hadi mafundo ya neva!’. Katika kufanya hivyo, Mshairi anamtarajia msomaji kusoma shairi lote kwanza, kama ilivyodokezwa kwa ishara [·] inayodai maelezo. Maelezo hayo ndiyo yanayotolewa katika mishororo inayofuata hadi mwishoni mwa shairi. Viakifishi hivyo vimetumiwa kwa makusudi ili hadhira iweze kufuatilizia kadhia kwa tuo huku ikisaili na kutafakari kila neno na kauli katika mishororo hadi ukingoni kulikotumiwa ishara

[!]. Kadhalika, mtunzi wa shairi ‘Wanafiki’ katika *Kichomi* (Kezilahabi, 1974: 24) ameandika ifuatavyo:

Wako wapi hoho! waliojidai mabikira?  
Haha! Wako wapi waliojidai utakatifu  
Watu hao wema wapole wako wapi  
Sifa wanayo, heshima hawana  
Mimba bendera, nyama hawali  
Jela viboko, udongo kusomba  
Miti kukata, mahindi kupanda  
Ai! Wako wapi wapenda ujamaa  
Waliokipiga kelele juzi? (ubeti wa 2)

Katika ubeti huo hapo juu, mshairi ametumia viakifishi vingi ikilinganishwa na shairi zima la ‘Machochi ya Damu’ katika *Bara Jingere*. Kama ilivyoelezwa hapo awali, viakifishi ni ishara ambazo hutumiwa siyo tu kama mbinu bali pia kama mtindo katika mashairi huru wa Kiswahili. Shairi moja huweza kuwasilisha maana inayoelea juu juu na maana batini. Kimsingi, lugha teule inayotumiwa katika uwasilishaji wa mashairi ‘yanayotajika’ ya Kiswahili huwa ni ya mshindo, kuvutia, kutafakarisha na kuliathiri sikio la hadhira. Kwa njia hiyo, ujumbe huwa si wa moja kwa moja bali huwa wa kiistiari au kimafulmo (Senkoro, 1988: viii). Aidha, mchakato huo wa ufasiri wa ujumbe katika mashairi huandamana na jinsi mtunzi alivyoakifisha utungo wake. Katika dondoo la ubeti uliopo hapo juu mshororo wa mwanzo umetumia viakifishi viwili: [!] na [?] (zaidi ya **HERUFI KUBWA** katika mianzo yote ya mishororo). Jinsi ambavyo vimetumiwa mwanzoni, vimepewa umuhimu katika ubeti huo. Isitoshe si kwa sadfa kwamba mtunzi ametumia [!] mara tatu katika sehemu za mwanzo za mishororo na [?] mara mbili katika mazingira yanayofanana. Kiashiria hicho cha ndani ya mishororo kinamtaraji msomaji kushangaa kwa yale anayoyasikia kupitia kwa mayowe ya mshairi. Katika viakifishi vya nje kina umuhimu wake katika kuibua mazingira ya kutotosheka na yale yaliyopo au yale yanayoendelea katika jamii. Swali hapa ni: Msomaji anahitaji kufanya nini ili kuweza kupata jibu linaloashiriwa na viakifishi cha [?] katika uhai? Hapa, msomaji anahitaji kupiga bongo na kujaribu kupata majibu kutokana na uhalisi wa maisha na utamaduni unaomwathiri. Kutokana na muda na nafasi aliyotengewa, mtunzi hana muda mwingi wa kufafanua hoja zake. Endapo hilo ni pengo, mtunzi huteua viakifishi ambayo atavitumia katika kuwasilisha mchomo wake wa ndani kwa ndani na kumhusisha msomaji katika usaili na utafakari wa ujumbe.

#### v. Dhima Nyinginezo za Viakifishi katika Mashairi Huru

Baadhi ya matumizi ya viakifishi katika ushairi huru wa Kiswahili yamefafanuliwa hapo awali katika makala hii. Kuna dhima nyinginezo ambazo zitatajwa hapa. Miongoni mwa dhima hizo ni: uelekezaji wa **toni na hali** katika mashairi; udhibiti wa mwendo katika usomaji na ughanaji wa kimoyomoyo au kwa sauti; kama chombo cha kubainishia mwelekeo na itikadi ya mtunzi; kama kielekezo cha ujenzi wa taharuki; udhibiti wa miundo ya mishororo na maumbo ya beti katika shairi; uelekezi katika

---

mahitaji ya mahadhi na ridhimu; kama mbinu ya usimulizi (utambaji) na kusemezana katika mashairi hayo. Hapa nitaeleza kwa kifupi kuhusu hizo kama ifuatavyo:

- **Kubainishia toni na hali** kutegemea tukio katika uwasilishaji wa mashairi huru ya Kiswahili. Hivyo, wizani husaidia sana wasomaji na wasikilizaji kwani hufungamana sana na maudhui. Ni mapigo yanayosaidia kuainisha mwendo wa shairi. Huu hapa ni ufafanuzi mfupi wa dhima hizo: viakifishi vinavyoweza kutumika katika mazingira ya furaha, ndoa, starehe na mapenzi ni [;], [,], [...] na [·]. Katika hali ya huzuni viakifishi vya usiyahi vinavyoweza kutumiwa ni [!], [?], [“ ”]. Matumizi hayo yanadhihirika kwenye shairi ‘Nimechoka’ katika *Kichomi* (kur. 34-35)

Machozi yananitoka, kujipangusa siwezi.

Najitahidi kutoa sauti kwa nguvu:

“Jamani e! Nisaidie! Ng’oeni hivyo vitimbo!”

Lakini wanadamu wanainama. Wanaanza sasa kusali. (Ubt. 4)

- **Udhibiti wa mwendo:** katika usomaji na ughanaji wa kimoyomoyo au kwa sauti. Kimsingi katika uwasilishaji wa ushairi mapigo ya silabi au mizani huwa ni kiumbiumbi cha nje katika kuainisha mwendo wa shairi. Kadhalika, kwa kuzingatia mashairi huru ya Kiswahili dhima hiyo pia hutekelezwa kupitia kwa viakifishi. Kama ilivyoelezwa hapo awali, **Herufi Kubwa** hutumiwa katika kuelekeza hadhira kutambua kuwa huo ni mwanzo au jina. Katika ushairi huru wa Kiswahili matumizi hayo huwa ya makusudi ili kuweza kusomwa kwa pumzi nyingi kama njia ya kuisitiza. Isitoshe, matumizi hayo huwa ni kidokezo muhimu cha mianzo ya kauli ngeni zaidi ya kuwa ni mianzo ya mishororo tu. Viakifishi vingine kama vile [“ ”], [...] [,], [;], [?], [!], [:] na [·] hutumiwa kwa makusudi katika mashairi huru kubainishia namna mishororo inavyoweza kusomwa na hadhira kama vile mtuo mdogo ndani ya mishororo; mshangao, swali au kuwa ndio mwisho wa mishororo au kuwa kiashiria cha kufikia ukingoni. Usomaji huwa wa matao ya chini ukilinganishwa na vile shairi lilianza kusomwa. Mfano hapa ni shairi ‘Flora na Wenzake’ katika *Bara Jingine* (uk. 33-36) imewasilishwa:

Waazi na wanafunzi

Humwita ‘Mwalimu\_ Mkuu’

Lakini jina lake halisi

Uoza! (ubeti wa 1)

Katika ubeti huo hapo juu, viakifishi hivyo ni vya kimsingi katika kuelekeza mahadhi yanayotarajiwa hasa kwa kuzingatia ridhimu na mwendo katika mishororo ya ubeti wa shairi kusudiwa. Kwa kuzingatia dondoo hilo ni kwamba kauli katika mishororo haziwezi kujisimamia pasi na kuhimidiwa kwa viakifishi mahususi hata kama kumetumiwa kauli na maneno teule inayochochea utafakari katika akili ya hadhira. Kupitia kwa matumizi ya viakifishi, mtunzi ameweza kuudhibiti mwendo na mahadhi katika usomaji wa shairi husika. Zaidi ya hayo, ametumia herufi kubwa kwa namna mbili: kama

mianzo ya mishororo na pia kama mbinu ya kudokezea hoja mpya katika shairi.

- **Viakifishi kama chombo cha kuelekeza mwelekeo na itikadi ya mtunzi.** Mtunzi wa fasihi, hususan wa ushairi wa Kiswahili anapowasilisha ujumbe, ujumbe huo huwa umetokana na tajriba yake na yale ambayo yamemwathiri. Hivyo, ushairi unakuwa kama jukwaa la kutolea hisi na mchomo wa msanii unaofungamana na itikadi yake ya maisha. katika uwasilishaji huo, mambo anayoyachukia au anayoyaona kuwa tege ndiyo humwelekeza katika matumizi ya viakifishi. Mifano kama hiyo ni kama ile inayopatikana kwenye shairi la ‘Hadithi ya Mzee’ katika *Kichomi* (1974: 69-72). katika shairi hili imewasilishwa:

Mara tukaona vimatu weusi  
Wengi wanarukaruka  
Kumbe wale nzige  
Waliacha mayai mchangani!  
Vimatu wanafufuka  
Kutoka mchangani  
Hao watoto wa nzige  
Au ni watoto wetu! (Ubeti wa 21)

Katika ubeti huu, sauti ya mtunzi inasikika kupitia kwa kuzinafsisha kauli zilizomo. Ingawa, ujumbe wa mtunzi umo katika kauli anazotumia, inajitokeza kwa uwazi zaidi kupitia kwa viakifishi vilivyotumiwa. Hivyo, alama ya [!] imetumiwa mara mbili katika ubeti huo siyo tu kuifanya matini kueleweka bali pia kuvishwa hisi za mtunzi kuhusu ujumbe unaowasilishwa. Mifano inayokariri mwelekeo wa mshairi ni katika mishororo ya ‘Waliacha mayai mchangani!’ na ‘Au ni watoto wetu!’ Katika mishororo hiyo, kiakifishi [!] kinaibua kejeli na kinaya katika kauli hizo zinazozingatiwa. Shairi ‘Mruko wa Nyuki’ katika *Bara Jingine* (kur.10-16) pia linadhihirisha suala lilo hilo la itikadi ya msanii ambapo imewasilishwa:

Ndotu yangu  
Ni tamu  
Kama asali,  
Kijani  
Kama majani ya mtango,  
Angavu  
Kama jua la asubuhi,  
Pendezi  
Kama bustani ya waridi;  
Ndotu-  
Ndotu ya bara jipya  
Bara ambapo  
Bunge  
Halitakuwa ukumbi

Wa genge la nzige, (uk. 10)

Katika dondoo hili mtunzi ameifumba itikadi yake kupitia kwa maneno teule ya ‘Ndoto yangu’, ‘Ndoto’, ‘Bara ambapo’ na ‘Bunge’. Kwa kiwango fulani, matumizi hayo yanadhihirisha tofauti za kimtindo katika uwasilishaji wa itikadi katika ushairi huu wa Kiswahili. Hata hivyo, katika shairi hili kumetumiwa [;] kwa njia mbili: kutofautisha na kushirikisha mawazo ya aina mbili kuhusu itikadi inayowasilishwa katika sehemu ya shairi hili.

**Hitimisho**

Katika uwasilishaji wa mashairi huru ya Kiswahili, viakifishi vina nafasi muhimu kama mbinu ya utunzi na uwasilishaji ujumbe. Vipengele hivyo huchangia vile vya kigrafolojia ili kuupa nguvu ya kimtindo katika kuuimarisha ushairi huru wa Kiswahili. Zaidi ya kutumiwa viakifishi kama mbinu ya kudhibiti viumbiumbi vya kisarufi katika usomaji wamatini kwa ujumla mashairi huru ya Kiswahili huwa na dhima ya kuwasilisha fikira na kujenga mahusiano ya usemezano baina ya mtunzi na hadhira. Kadhalika, matumizi hayo huelekeza usomaji wa kimantiki unaojenga mshikamano wa hoja kuanzia mwanzo hadi tamati. Mashairi ya Kiswahili yanayozingatia mno arudhi za uwasilishaji, hutumia viakifishi kama mbinu ya kuidhibiti miundo ya ndani kwa ndani. Kadhalika, viakifishi hivyo huweza kutabiriwa na msomaji. Katika mashairi huru ya Kiswahili, viakifishi hutumiwa kwa makusudi kama mtindo wa uwasilishaji; kudhibiti miundo ya ndani kwa ndani na kwenye kingo za mashairi; uwasilishaji wa ujumbe unaojikita kwenye hisi za mtunzi na itikadi ya mtunzi; kuelekeza usomaji wa kimoyomoyo au ughanwaji wake.

Aidha, viakifishi katika enzi ya sasa vinatekeleza dhima ya mihemko ya kihisia, ishara za mghanaji, ridhimu na mahadhi yanayohusishwa zaidi na ushairi katika kitengo cha simulizi. Hivyo, matumizi ya viakifishi ni njia muhimu katika uhifadhi wa mbinu za uwasilishaji wa ushairi huo simulizi uliokuwa na umekuwa ukienziwa katika mapokeo ya jamii mbalimbali za Afrika Mashariki. Katika kuzingatia matumizi ya viakifishi katika ushairi wa Kiswahili, kuna uwezekano wa kuanisha mashairi hayo kimakundi: yanayotumia viakifishi vya ndani kwa ndani; yanatumia katika pembezo; yanayotumia viakifishi mahsusi kama viashiria vya ndani ya beti au katika shairi zima kama mbinu ya kuibulia hisi na namna vinavyochangia uhuru wa usemezano katika shairi. Aidha, kuna haja ya kuendeleza utafiti kwa kuzingatia namna viakifishi vinavyotumiwa kama njia ya kubainishia umaarufu wa kimtindo na kimuundo katika uwasilishaji wa mashairi.

**Marejeleo**

- Abdalla, A. (1973). *Sauti ya Dhiki*. Nairobi: Oxford University Press.
- Alembi, E. (2000). *Understanding Poetry*. Nairobi: Acacia Publishers.
- Barth, J. (1984). *The Literature of Replenishment*. London: John Hopkins University Press.
- Harries, L. (1962). *Swahili Prosody*. Oxford: Clarendon Press.
- John, M. (1990). *Punctuation For Now*. London: Palgrave Macmillan Press Ltd.
- Leech, G. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman.
- Leech, G. N. na Short, M. H. (1981). *Style in Fiction, A linguistic introduction to English Linguistics*. University of Texas at Arlington.
- Macgoye, M. O. (2009). *The Composition of Poetry*. Nairobi: Univesity of Nairobi Press.
- Masinde, E. W. (2007). *Ufundishaji wa Ushairi wa Kiswahili katika shule na Vyuu*. Eldoret: Taaluma Publishers.
- Mazrui, A. (1988). *Chembe cha Moyo*. Nairobi: Heinemann Kenya Ltd..
- Mboya, T. M. (2000). *How to find meaning in a Poetry*. Eldoret: Western Educational Publishers.
- Mohamed, S. A. (2002). *Jicho la Ndani*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.
- Mulokozi, M. M. na Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Ramadhani, J. (1973). "Ushairi" katika *Mulika Na. 3*. Dar es Salaam: TUKI.
- Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Wafula, R. M na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Wanjala, F. S na Kavoi, J. M. (2013). *Stadi za Mwasiliano na Mbinu za Kufundisha Kswahili*. Mwanza: Serengeti Bookshop.